## LIFAHAMU KANISA LA WAADVENTISTA WASABATO TANZANIA.

Utafiti uliofanyika, unaonyesha kuwa vijana wengi hawaifahamu historia ya kanisa la Waadventista wasabato. Baadhi ya sababu zinazochangia vijana kutolifahamu kanisa lao ni pamoja na.

- Vijana wengi ni wachanga wa imani. Wanapobatizwa, wanafahamu mambo machache tu.
- Kozi hii hutolewa na idara ya vijana pekee, na vijana wengi hawako katika idara ya vijana. Kutojiunga na idara ya vijana kunawafanya wabaki gizani muda wote.
- Kuridhika na nuru ndogo waiyokwisha ipokea.

**Kwanini tunahitaji kuifahamu historia ya kanisa la Waadventista Wasabato Tanzania?**

- Itatusaidia kujua namna Mungu alivyotuletea nuru hii kupitia Wamishenari mbalimbali waliotoka Ulaya.
- Itatusaidia kujua jinsi Mungu alivyoliongoza kanisa hili hadi kufikia hapa tulipo.
- Itatusaidia kutuongezea imani na kutujengea uwezo wa kuitetea imani ya utunzaji wa sabato kwa gharama yoyote.
- Itatupatia maarifa ya kurithisha kwa vizazi vijavyo kama Yesu atachelewa kurudi.

## JINSI KANISA LA WAADVENTISTA WASABATO LINAVYOJULIKANA

Kanisa la Waadventista Wasabato, linajulikana kwa jina la Unabii kuwa “**Kanisa la Masalio**”

(Isa 10:20-22, Rum 9:27,

Katika kamusi ya Kiingereza ya “Oxford Dictionary”, uk.992 inasema “Remnant –That is left after the other parts have been used or destroyed…

**Je, kanisa hili limesalia kutoka wapi?**

- Limesalia kutoka katika makanisa yaliyoiangusha kweli chini na kuingiza mapokeo (Makanisa ya Babeli)
- Limesalia katika kutembea kwenye mapito ya zamani ya neno la Mungu (Yer
- Limesalia katika kuuhubiri ujumbe wa malaika watatu (Uf 14:6-12)
- Limesalia katika utunzaji wa amri za Mungu ikiwemo na sabato ya siku ya saba. (Kut 20:1-17, Uf 14:12)

## CHIMBUKO LA KANISA LA MASALIO

Kanisa hili limetokana na utimilifu wa unabii wa Math 24:29-30. Watu wa Mungu walianza kulinganisha unabii huu na matukio yafuatayo:

- Tetemeko la Lisbon. -1755

- Jua kutiwa giza- May 19,1780
- Kuanguka kwa nyota-1833

Baada ya matukio haya, kulitokea uamsho mkubwa kule Marekani (Great Awakening). Watu walianza kusoma Biblia kwa bidii na kuyalinganisha matukio haya na kuja kwa Yesu mara ya pili. Vikundi mbalimbali vya uamsho na matengenezo vilianzishwa kule Marekani na Ulaya. Kule Marekani kulianzishwa kundi kubwa la uamsho lililoongozwa na ndugu William Miller. Yeye alitoka katika kanisa la Baptist. Alisoma unabii wa kutakaswa kwa patakatifu wa Dan 8:14. Aliamini kuwa patakatifu ni hapa duniani, ambapo kwasasa pamechafuliwa na dhambi, na hivyo Yesu anakuja kupatakasa na kukomesha dhambi.

Alipofanya hesabu ya siku 2,300 za kutakaswa kwa patakifu, aligundua kuwa siku hizo zinaishia katika tarehe 22, Oktoba 1844. Akatangaza msimamo wa imani yake ya kwamba Yesu atakuja kutakasa dunia mwaka 1844. Ujumbe huu ulipokelewa na watu wengi kule Marekani. Wengi walijiandaa kumpokea Yesu katika mwaka 1844. Wengine walitengwa na makanisa yao kwajili ya msimo wao. Ujumbe hu wa William Miller, uliwaandaa Watu wapatao 50,000 kwa ujio wa Yesu. Hawa walikuwa Waadventista wa kwanza lakini hawakuwa wasabato.

**KUKATA TAMAA KUKUBWA**. (The great disappointment)

Yesu hakurudi katika mwaka 1844 kama yalivyokuwa matarajio yao. Wengi walikata tamaa. Wengine walirudi katika makanisa yao ya zamani. Wachache waliendelea kuchunguza kwa bidii na kwa maombi mengi ili kujua ni wapi walipokosea. Walirudia tena zile hesabu zao. Wakaona kuwa ziko sahihi. Wakaendelea kuomba ili Mungu awaonyeshe mahali kosa lilipotokea. Miongoni mwao alikuwemo Hiram Edson, Joseph Bates, Ellen Harmon, James white, Fredrick Wheeler, na Rachel Preston.

Siku moja Hiram Edson alipata njozi katika shamba la ngano mahali alipokuwa amezoea kufanyia ibada. Hapo alipata njozi ya pekee. Alionyeshwa Yesu anatoka katika chumba cha patakatifu pa kwanza tarehe 22 Oktoba, 1844 na kuingia katika chumba cha patakatu pa pili kwaajili ya kuendesha hukumu, na ndipo atakuja kuwachukua watu wake. Njozi hii iliwafanya kutambua kuwa hesabu zao zilikuwa sahihi. Kasoro ilikuwa katika kutafsiri.

Kundi hili lilitiwa moyo na majibu ya maombi yao. Walizidi kuendelea kuchunguza maandiko kwa maombi mengi ili Roho wa Mungu aendelee kuwafunulia nuru nyingine ambayo walikuwa hawajaifahamu bado. Ndipo Mungu akawafunulia utunzaji wa sabato ya siku ya saba yaani jumamosi. Baada ya kupata nuru hii, kundi zima likakata shauri kuanza kutunza sabato ya siku ya saba yaani jumamosi. Takribani watu wapatao 40 ndio walioamua kutunza sabato huku wakingoja marejeo ya Yesu.

## KUONGEZEKA KWA KUNDI LA WANA MAREJEO WATUNZA SABATO

Nuru hii ya utunzaji wa sabato na kusubiri kurudi kwa Yesu mara ya pili ilizidi kupokelewa na watu wengi. Makundi ya wana marejeo watunza sabato yalizidi kuongezeka kule Ulaya na Marekani. Jambo hili lilipelekea kuanzisha mfumo maalum wa kuongoza kundi hili.

- Kulihitajika viongozi wa kusimamia kundi
- Kulihitajika wahazini watakaotunza mali na thamani za kanisa.
- Kulihitajika kupata mafundisho makuu ya imani yanayowaunganisha kiimani.
- Kupata jina litakalowatofautisha na watu wa imani nyingine.

Jambo hili lilionekana kuwa ni zuri machoni pa watu, ingawaje wengine walilipinga, wakiamini kuwa na mfumo kama huo nikupatana na ulimwengu. Ellen Harmon, ambaye baadaye aliolewa na Jamea White alisaidia sana kuelekeza juu ya jambo hili la kuwa na mfumo. Mungu alimpatia maono yafuatayo: - “Kuna utaratibu mbinguni, na Mungu anafurahishwa na juhudi za watu wake za kuanzisha mfumo wa utaratibu kwa ajili ya kazi yake hapa duniani… Nilionyeshwa kwamba ni lazima kuwe na utaratibu katika kanisa la Mungu; na mfumo huo unahitajika ili kupeleka mbele ujumbe wa mwisho wa rehema katika ulimwengu. (1T uk 191, Church Heritage uk. 41)

Mwaka 1860 walikubaliana kuanzisha jina la dhehebu ambalo litatambulikana rasmi kisheria. Majina kadhaa yalipendekezwa. Kwa msaada wa E.G.White jina la Seventh day Adventist church (SDA) lilipitishwa. Nabii wa Mungu alionyeshwa kuwa; “Jina la Seventh day Adventist church limechukua amali zote za ukweli wa imani yetu.” 1Tuk 224. Mwaka 1963, General Conference ya kwanza ilikutana na kupitisha rasmi jina la Seventh day Adventist church. (SDA)

Wakati huo kulikuwa na mafundisho makuu ya imani 9. Kulikuwa na washiriki 3,500 na makanisa 125. Wachungaji waliowekewa mikono walikuwa 22. Wachungaji walei walikuwa 8. Kwa sasa, kanisa linawaumini katika nchi zipatazo 204 kati ya nchi 230 zinazotambuliwa na umoja wa mataifa. Hadi sasa, kanisa lina waumini takribani wasiopungua milioni 14 ulimwenguni.

## VITAMBULISHO VYA KANISA

### 1.<u>Jina la kanisa</u> (Seventh day Adventist church)

Kwa kiswahili ni Waadventista Wasabato. Jina hili hutambulisha kuwa hawa ni watu wanaongoja kuja kwa Yesu mara ya pili huku wakitunza sabato ya siku ya saba yaani jumamosi.

Waadventista wengi wanapatikana Amerika kaskazini, kati na kusini, Austaria, Ufilipino, Afrika kusini, Afrika mashariki, na Afrika Magharibi.

2. **Misingi ya imani**

**Kanisa lilianza kwa kuwa na misingi ya imani 9. Misingi hii iliendelea kuongezeka kulingana na nuru ilivyopanuka pamoja na mahitaji ya kanisa, kulingana na utimilifu wa unabii. Leo hii kanisa lina misingi 28. Misingi hii imegawanyika katika makundi makuu 6 kama ifuatavyo:**

1. Mafundisho yanayomhusu Mungu.
2. Mafundisho yanayomhusu mwanadamu.
3. Mafundisho yanayohusu wokovu wa mwanadamu.
4. Mafundisho yanayohusu kanisa.
5. Mafundisho yanayohusu maisha ya kikristo.
6. Mafundisho yanayohusu matukio ya siku za mwisho.

3. **Nembo ya kanisa.**

Kwa muda wa takribani miaka 150, kanisa halijawahi kuwa na nembo rasmi ya kulitambulisha kanisa. Kila nchi ilibuni nembo yake. Baraza kuu la ulimwengu lililokutana mwaka 1996 lilipitisha rasmi nembo itakayolitambulisha kanisa la Waadventista Wasabato ulimwenguni. Nembo hiyo imejaa vielelezo vinavyowakilisha misingi ya imani.

**VIELELEZO VYA NEMBO YA KANISA LA WAADVENTISTA WASABATO**

1. **Biblia iliyo wazi**: Waadventista Wasabato tunaamini kwamba neno la Mungu pekee ndio msingi wa wokovu wa maisha ya wanadamu. (2Tim 3:16)
2. **Miale ya moto:** Mistari mitatu ya miale ya moto huwakilisha ujumbe wa malaika watatu. (Uf 14:1-12). Ujumbe huu wa malaika watatu hupelekwa kwa nguvu ya uongozi wa Roho Mtakatifu.
3. **Msalaba:** Kanisa la Waadventista Wasabato huamini kwamba Kafara ya Kristo ndiyo kiini cha ukombozi wa maisha ya mwanadamu. (Mdo 4:12, 1Kor 3:11, 2:1-2, 1Kor 5:7, Gal 6:14, Nyimbo za Kristo 120.
4. **Ramani ya ulimwengu:** Waadventista Wasabato huamini kwamba injili ya marejeo ya Yesu ni lazima ihubiriwe katika ulimwengu wote. Hilo ni agizo la Yesu ambalo kanisa limepewa (Math 28:19,20)

## KUINGIA KWA KANISA LA WAADVENTISTA WASABATO TANZANIA

Katika mwaka 1903, **Ludwig Richard Conradi** (Mjerumani), aliyekuwa kiongozi wa kazi kule kule Ujerumani, aliwiwa sana kuileta imani hii ya Kiadventista huku Afrika Mashariki. Wakati

huo, idadi ya washiriki ulimwenguni ilikuwa takribani 77,554. Kati ya hao washiriki wapatao 9,547 walikiuwa Ulaya.Ujerumani peke yake ilikuwa na Waadventista wapatao 3,400.

**Ludwig Richard Conrad** alihamasisha washirki wa Ujerumani wakachanga fedha zenye thamani ya dola 5,000 kwaajili ya kutuma wamishenari Afrika Mashariki. Kanisa la Ujerumani liliwachagua wamishenari wawili, ndugu **A.C Enns** na **Johanes Ehlars** kuja kuleta injili ya Kiadventista Afrika Mashariki. Ndugu A.C Enns alikuwa **mkulima wa bustani ya mboga** aliyechukua **stashahada ya uchungaji** katika **chuo cha Friedensau** huko Ujerumani. Ndugu Ehlars alikuwa ameajiriwa kama **fundi wa kupaka rangi majengo ya misheni** kule Ujerumani.

Walmishenari hawa, **walianza safari yao ya kuja Afrika Mashariki tarehe 22 Oktoba, mwaka 1903**. Ehlars alikuwa amemwoa Ester. Kwa sababu ya kujitoa kwake kuja Afrika Mashariki, alilazimika kutengana naye. Enns, alikuwa ana mchumba ambaye ilimlazimu kutengana naye pia. **Novemba 9**, walifika katika **pwani ya Mombasa** wakiwa na barua ya kuja Tanganyika. Gavana wa Mombasa aliwaelekeza ramani ya kuja pwani ya bandari salama (Dar es Salaam), ambapo **walisafiri muda wa siku tatu hadi kufika Dar es Salaam**. Walipofika Dar es Salaam, walipokelewa na Gavana wa Ujerumani wa Tanganyika. Aliwaalika rasmi kwa chakula cha jioni ofisini kwake. Wamishenari hawa wawili walipata nafasi ya kumweleza sababu ya wao kuja Tanganyika. Kwakuwa **pwani ya Dar es Salaam ilikuwa tayari ina Waislamu na baadhi ya madhehebu ya Kikriso**, aliwaelekeza waende katika **milima ya upare kusini ambako hakukuwa na dhehebu lolote.**

Wamishenari hawa **walisafiri kwa treni kupitia Tanga hadi wakafika Korogwe**. Kutoka Korogwe, **walisafiri kwa miguu hadi walipofika GITI** na kuamua kufanya makao yao hapo Giti. **Tarehe 25 Novemba 1903 walituma ujumbe kwa njia ya simu kuwa wamefika salama Tanganyika na wamepewa eneo la Pare kusini** na Gavana wa serikali ya Kijerumani. Hapo Giti, **walinunua ekari 25 toka kwa chifu Sekimanga, ambapo wali mpatia rupia 100.**

Ubatizo wa kwanza ulifanyika mwaka 1908, ambapo Waadventista wa kwanza wapato 6 walibatizwa. Majina yao ni:

1. Andrea Senamwaye.
2. David Masumba Chambega.
3. Abrahamu Salimu Seivunde.
4. Yohana Kajembe
5. Philipo Mmbaga
6. Lazaro Omari.

Baadaye, wainjilisti wachache miongoni mwa hawa waliobatizwa walitumwa kwenda kanda ya ziwa. Wakaanzisha misheni yao kule Bupandagila.

## VITA KUU YA KWANZA. MPAKA MWAKA 1960

Vita kuu ya kwanza ilipotokea, ilisababisha wamishenari wa Kijerumani waliokuwa wamekuja kuanzisha kazi Tanganyika kukimbia na kurudi kwao. Jambo hili lilihafifisha kwa kiwango kikubwa cha ukuaji wa Uadventista. Baadaye kanisa lilituma Wamishenari toka Uingereza ili kuja na kuendeleza kazi iliyoanzishwa na wamishenari wakijerumani. Walipokuja, walianzisha vituo maalum vya misheni kule Ikizu, majita, Bupandagila na Utimbaru. Kule Upareni, kituo cha Giti kilihamishwa na kupelekwa Suji.

Baadaye shule ya sekondari ya wasichana ikaanzishwa kule Bupandagila. Mwalimu wa kwanza wa Tanganyika wa cheti cha ualimu alitokea Suji. Aliitwa kwa jina la Damari Kangalu. Wachungaji wa kwanza kuwekewa mikono, walikuwa Paulo Kilonzo na Elisa Manongi. Waliwekewa mikono katika mwaka 1932. Hawa wote walitokea Upare Kusini.

## KUENEA KWA IJNILI YA WAADVENTISTA WASABATO KATIKA MIJI MIKUBWA.

Mikutano mikubwa ya injili iliyojulikana kama “Mashambulio” ilifanyika katika miji ya Arusha, Moshi, Mwanza, Dar es Salaam, Morogoro na Iringa katika mwaka 1960. Wamishenari waliofanya mikutano hiyo ya mashambulio walikuwa mwinjilsti Bendana Cleveland, wakisaidiana na Watanzania ambao ni Mwinjisti Pr. Fares Muganda, Pr. Gabriel Mbwana, Pr. Elizafan Wanjara na Pr. Nyagabona.

## MATUKIO MUHIMU KATIKA HISTORIA YA KANISA LA WADVENTISTA WASABATO TANZANIA

| MWAKA | TUKIO |
|---|---|
| 1903 | Wamishenari wa kwanza walifika Tanganyika. |
| 1908 April 4 | Ubatizo wa kwanza ulifanyika huko Giti, wakiwemo wanafunzi 6 wa ubatizo |
| 1909 | Kituo cha Busegwe kilianzishwa na E.C Enns. |
| 1909 | Kituo cha majita kilianzishwa. Kanisa kubwa la kutosha watu 600 lilimalizika mwaka 1911. |
| 1910 | Kituo cha Ikizu wakati huo kiliitwa Kidzo kilianzishwa. Kilianza kama middle school, na baadaye kikawa chuo cha ualimu. |
| Des. 1911 | Ubatizo wa kwanza ulifanyika kule Majita, na watu wawili walibatizwa ambao ni Yohana Mtarimbo (Mjita) na Philipo Kayanda (Msukuma) |
| 1913 | Watu wengine 52 walibatizwa. Ulikuwa ubatizo wa kikistoria ambao haukuwahi kutokea |
| 1913 | Wamishenari wanne walitumwa kwenda Usukumani. Majina yao ni Isaya Fue (Alikwenda Kanadi), Petro Mlungwana (Alikwenda Unyantuzu), Danieli mwenda (Alikwenda Itilima), Philipo Sekisago (Alikwenda Mwagala) |
| 1915 | Kulitokea vita kati ya Wasukuma na Wamasai. Mmishenari wa Kijerumani aliuawa |

| | |
|---|---|
| | kule Kanadi alipokuwa akijaribu kuwaokoa rafiki zake wa Kisukuma dhidi ya Wamasai. |
| 1916 | Vita kuu ya kwanza ilikuwa imepamba moto, na wamishenari walikimbia kurudi kwao. Hali ya kanisa ilikuwa mbaya. Wazee wa kanisa waliteuliwa na wamishenari kulisimamia kanisa. Daniel Tendwa(Giti), Petro Sebughe(Suji), Ezekiel Kibwana (Kihurio), Abraham Msangi (Vunta) |
| 1917 | Wamishenari wengi wa Ujerumani walikamatwa na kurudishwa Ujerumani. |
| 1917 | Waingereza walizikataa huduma za Waadventista kuendelea kutolewa hadi mwaka 1920 waliporuhusu huduma hizo ziendelee tena. |
| 1924 | Wamishenari Harry na Ada Rabson waliwasili Bupandagila. Walitumika hapo hadi mwaka 1940. Mrs Rabson alifungua zahanati iliyovuta wagonjwa wengi kutoka pande za usukumani. |
| 1926 | Makambi ya kwanza Tanganyika yalifanyika huko Mamba Myamba (Upare) |
| 1929 | S.G. Maxwell ndiye mmishenari wa kwanza wa Kiingereza kutumwa Tanganyika. Aliwasili mwaka 1929 |
| 1927 | Walimu wa kwanza wa Kisabato walitunukiwa vyeti huko Suji |
| 1929 | Chuo cha ufundi kilianzishwa huko Suji. Masomo yaliyotolewa yalikuwa katika fani za uashi, useremala, ushonaji na ufundi viatu |
| 1930 | Shule ya wasichana ya Ntusu ilianzishwa na mmishenari aitwaye Lucy Clarke |
| 1931 | Damari Kangalu alihitimu masomo ya ualimu huko Suji na kutunukiwa cheti cha serikali. Alikuwa mwanamke wa kwanza hapa Tanzania kutunukiwa cheti hicho. |
| 1933 | Mmishenari Rudolf Ruder alifanya kazi kule Majita. Akatafsiri agano jipya kwa lugha ya Kijita. Alikichapa katika mwaka 1943. |
| 1933 | Ubatizo wa kwanza ulifanyika katika kisiwa cha Ukerewe. Watu wapatao 59 walibatizwa. Waliandaliwa na Mwinjisti Petro Mugunda aliyejitolea kwa hiari bila kutumwa na kanisa. |
| 1932 | Watanzania wa kwanza wachungaji waliwekewa mikono. Hawa walikuwa Elisa Maningi Kilonzo na Paulo Saburi Kilonzo |
| 1934 | Watu 186 walibatizwa kule Majita. |
| 1935 | Kanisa la Mamba Myamba lilifunguliwa. Lilijengwa mwaka 1932 kwa nguvu za washiriki. |
| 1936 | Chuo cha ualimu Ikizu kilitambuliwa na serikali na kikaanza kupata misaada ya serikali. |
| 1938 | Makambi ya kwanza Tanganyika yalifanyika kanda ya ziwa. |
| 1945 | Ikizu ilikuwa middle school pekee ya Waadventista Wasabato iliyosifika na kuvuma nchi nzima. |
| 1947 | Kazi ya ujenzi wa hospitali ya Heri ilianza. Hospitali hii ilianza kazi mwaka 1949. |
| 1952 | Idara ya uchapaji nchini ilianzishwa, na mchungaji Fares Muganda alichaguliwa kuwa mkurugenzi wa kwanza wa uchapaji. |
| 1962 | Paulo Bomani alikuwa Mwadventista wa kwanza kuwa waziri katika serikali ya Tanganyika. |

## USAJILI WA KANISA LA WAADVENTISTA WASABATO TANZANIA

Tangu kanisa la Waadventista Wasabato lilipoanza Tanzania mwaka 1903, lilikuwa linafanya kazi ya kueneza injili ya marejeo ya Yesu bila kusajiliwa rasmi, kwa takriba ya miaka 51. Kuchelewa kulisajili kanisa kulitokana na sababu kuu mbili.

- Viongozi hawakuona haja ya kulisajili kwa vile hawakuwahi kupata shida na Serikali.
- Kwa mujibu wa nuru ndogo waliyokuwa nayo, wengine waliamini kuwa, kulisajili kanisa serikalini ni sawa na kuungana na ulimwengu.
- Wengine waliamini kuwa Yesu anakuja haraka, kwa hiyo hakuna haja ya kulisajili kanisa.

Kadiri miaka ilivyozidi kwenda, nuru iliendela kukua. Haja ya kulisajili kanisa serikalini ilizidi kuwa kubwa.

## SABABU ZA KULISAJILI KANISA LA WAADVENTISTA WASABATO TANZANIA

- Kuliwezesha kanisa kuendesha shughuli zake kwa kutambuliwa na Serikali, na hivyo kuwa na uhalali kisheria wa kuwepo kwa kanisa. Mfano kupewa kibali cha kuhubiri
- Kuwa na haki ya kisheria ya kumiliki raslimali za kanisa ikiwemo ardhi, shule, zahanati, kufungua Account bank, n.k.

Kanisa linaposajiliwa, linasajiliwa kwa mujibu wa sheria iliyomo katika nchi husika, na siyo matakwa ya kanisa husika. **Kwa mara ya kwanza kanisa la Waadventista Wasabato lilisajiliwa kwa sheria ya nchi ya Tanganyika mwaka 1954.** Lilisajiliwa kama "**British Adventist Mission Limited**". Ilikuwa wakati wa utawala wa Mwingereza.

Katika **mwaka 1960 Julai 21**, sheria ya usajili ilibadilika. Kanisa likasajiliwa kwa jina la "**Seventh day Association of South Africa**". Baadaye, sheria ya usajili ilibadilika. **Tarehe 23 Feb, mwaka 1999**, kanisa likasajiliwa kwa jina la **"Seventh day Adventist Association kwa namba ya usajili "SO. 5333"**. Hadi leo, kanisa limesajiliwa kwa jina hili.

Neno Association humaanisha ushirika, au umoja, hivyo serikali inaposajili Seventh day Adventist Association, humaanisha **"Umoja wa makanisa ya Waadventista Wasabato Tanzania**". Makanisa mengine pia yamesajiliwa kwa sheria hii ya Association. Kwa mfano Free Pentecoste Association, Baptist Association, Association of Lutheran churches of Tanzania, Association of Menonite churches of Tanzania, nk.

Kwasababu ya kuwa na usajili huu, tumeruhusiwa kuwa na raslimali tunazomiliki kama

- Taasisi za elimu, afya, uinjilisti, mawasliliano, n.k

- Mashamba ya kilimo na mboga mboga. mfano Kibidula
- Ardhi na majengo mbalimbali
- Kuendesha mikutano ya injili. n.k

**ORODHA YA VIONGOZI WALIOLIONGOZA KANISA LA WADVENTISTA WASABATO**

Tangu mwaka 1933, Tanzania iliitwa **"Tanganyika Mission Field"**. Kabla ya mwaka huo, Tanganyika likuwa na field mbili zifuatazo:

1. Field ya Upare iliyojulikana kama "East Tanganyika Mission".
2. Field ya Mwanza iliyojulikana kama "West Tanganyika Mission"

Tangu mwaka 1960 Tanganyika ilikuwa Union Mission. Wafuatao walichaguliwa kuwa viongozi wa kazi ya Bwana.

| MWAKA | MWENYEKITI | MWAKA | MAKATIBU | WAHAZINI/MAKATIBU |
|---|---|---|---|---|
| 1933-1936 | G.A. Ellingworth | 1933-1935 | | Mrs. M. Ellingworth |
| 1937-1939 | A. Sprogis | 1938-1940 | | R. Reinhard |
| 1939-1940 | H. M. Sparrow | 1941-1942 | | G. Pierson |
| 1943-1946 | F. H. Thomas | 1943-1954 | | H. Robson |
| 1947-1950 | H.E. Kotz | 1955-1960 | | M.W. Cuthbert |
| 1951-1955 | F.G. Raid | 1961-1965 | | R.D Marx |
| 1956-1958 | J.D. Harcombe | 1966-1968 | | E.G. Olsen |
| 1959-1963 | C.T.J Hyde | 1969-1975 | S.D. Otieno | H. Salmann |
| 1963-1965 | F.G. Thomas | 1975-1990 | E. Okeyo | H. Zerai |
| 1966-1969 | P.G. Werner | 1990-1991 | | D. Kihogo |
| 1970-1975 | L.C. Robinson | 1992-2000 | W. Mutani | A. Manyama |
| 1975-1980 | D. Biedsell | 2002-2010 | B. Mambwe | Z. Rabieth |
| 1980-1985 | Yohana Lusingu | 2011- | D. Fue | D. Wairaha |
| 1986- | R.W. Taylor | | | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1990 | | | | |
| 1990-1998 | N.L. Mwamukonda | | | |
| 1998-2002 | Geofrey G. Mbwana | | | |
| 2002-2005 | Steven Binna | | | |
| 2006-2010 | Joshua K. Kajula | | | |
| 2011- | Godwin Lekundayo | | | |